

KARIBU MWENGE WA UHURU 2018 WILAYANI KWETU TANDAHIMBA

Haya Hayaaa,Tandahimba Kuchelee Mwenge wa Uhuru 2018 huooooo!!!!

Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba Mhe. Sebastian Waryuba anawatangazia wananchi wote kuwa kutakuwa na ujio wa Mwenge wa Uhuru 2018.

Mwenge wa Uhuru utaingia wilayani Tandahimba siku ya tarehe 16.06.2018 na utapokelewa katika kijiji cha Lidumbe Mtoni ukitokea Wilaya ya Newala.

Baada ya kupokelewa Lidumbe Mtoni Mwenge Utaenda kuzindua ujenzi na ukarabati wa majengo ya kituo cha afya Mahuta na baadae utaenda kuweka jiwe la msingi madarasa mawili sekondari ya Nanhyanga na kuweka jiwe la msingi ujenzi wa stendi Nanhyanga ambapo ujumbe wa Mwenge utatolewa hapo.

Mwenge ukitoka Nanhyanga utaenda Malopokelo ambapo utazindua mradi wa nyumba sita za walimu sekondari ya Tandahimba na baadae utaenda kufungua kituo cha ufundu stadi shule ya Msingi Matogoro.

Mwenge ukitoka Matogoro utaenda kufungua Bweni moja la wasichana shule maalum ya Mji Mpya na baadae utaenda katika ukumbi wa halmashauri ambapo kutakuwa na maonyesho ya wajasiriamali na ujumbe wa Mwenge kutolewa kwa wananchi.

Mwenge ukitoka ukumbi wa halmashauri utaenda Nachunyu na utaweka jiwe la msingi ujenzi wa vyumba viwili vyta madarasa sekondari ya Nachunyu na baadae Mwenge utaelekeea Luagala kupitia Mkonjowano ambapo utaweka jiwe la msingi matundu 32 ya vyoo,kufungua ujenzi wa kisima cha kuvunia maji ya mvua lita laki moja (100,000) na kuangalia ukarabati wa shule ya msingi Luagala na mwenge utalala hapo hapo Luagala.

Siku ya pili ya tarehe 17.06.2018 Mwenge wa Uhuru utaondoka Luagala saa 1.00 asubuhi kupitia Mkonjowano, Nambahu na kukabidhi halmashauri ya wilaya ya Nanyamba katika kijiji cha Chikwaya.

Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba anawaomba wananchi wote kujitokeza kwa wingi kuupokea Mwenge wa Uhuru 2018 wenye kauli mbiu isemayo

“Elimu ni Ufunguo wa maisha,Wekeza sasa kwa maendeleo ya Taifa letu”

Tangazo hili limetolewa na

Mhe.Sebastian Waryuba

MKUU WA WILAYA YA TANDAHIMBA